# Kukumbuchila

## Chilongole

Chitabu cha Kukumbuchila ndo kuhiluchila kwa malajizo galingulongwa kulavigwa mgati mwa chitabu viyage vya Malajizo (vitabu vihano vya mwaluko kuli Ilagano lya Katali). Itagwa lya Chiebulaniya lya chitabu achi lina itagwa lya mina “Ulonzi.” Yangukundigwa kota Musa ndo yandichile chitabu achi ila honhu hado ha kuduma hangulonga mbuli za kubagama kwa heye. Chitabu achi changwaluka na ulonzi ulingulonga, “Awu ndo ulonzi wa Musa woyawalonjele Isilaeli.” Vitabu vya Ilagano Linyale vyangukunda kota Musa ndo yandiche chitabu cha Kukumbuchila. Petili loyasomile kulawa kuli chitabu cha Kukumbuchila 18:15-18, nakalonga kota awu nawali ulonzi wa Musa (Madito 3:22-23). Musa yoweza kuwa nakandika chitabu cha Kukumbuchila hamwe na vitabu vya Mwaluko na Kulawa na Walawi na Hisabu kuli hagati ha miyaka 1400 ama 1300, Kilistu loyang'hali kupondigwa.

Chitabu cha Kukumbuchila nachandichigwa kota ilagano lya mndewa na isi iwele hali ulongozi wake, kota vyoiwele aho katali. Ndo ilagano lya Nguluwi na Waisilaeli. Nguluwi nakakunda kuwatambichiza wanhu wone wahawinzile na kibatilila malajizo ga heye. Wone Waisilaeli wahabelenhuche mizilo ja Nguluwi, lelo wahagazigwe. Ayi yangulajilwa kuli chila honhu ha chitabu achi, ila sula ya 27 na ya 28 zangulonga kukomya.

Zilonga utambichizo na upanjilo viwele vyahawezile kulawila kwa chiwalo cha kuhulichiza ama kubelenhuka kwa Waisilaeli. Nhanzi za Isilaeli nazima hali vidunda vili vimile vilingilola na kilonjela utambichizo awu na upanjilo kota nzila ya kutawiza ilagano.

**Gali mgati**

1. Kuli sula ya 1-3 Musa kangulonga galawile kuli majendo ga Isilaeli kuloka chiwala.
2. Sula ya 4-26 zangusimila malajizo ga ilagano lya Nguluwi na wanhu wa heye.
3. Hamba kuli sula ya 27 mbaka ya 30 Waisilaeli wangulonga utambichizo na upanjilo kwa lizi ng'hulu kulajila kota kulawa mhela wula ilagano nalyali litawizwe.
4. Kuduma, kuli sula ya 31-34 Musa kangulonga ulonzi wa kuduma kwa Yoshua na kwa chila nhanzi ya Isilaeli loyawele yang'hali kubagama.

### *Ilajizo lya kuka kuli chidunda cha Holebu*

1 Chitabu achi china ulonzi uwele Musa
nakawalonjela wanhu weng'ha wa Isilaeli mhela
lowawele mchiwala kolilawilaga isanya mwa
lwanda lwa Yolodani. Nawali hali ibindi lya
Yolodani behi na Sufu, hagati mwa muji wa
Palani ubanzi umwe na muji wa Tofeli na Labani
na Haseloti na Disahabu ubanzi wunji. 2 Ndo
majendo ga mazuwa kumi na imwe kulawila
kuchidunda cha Holebu mbaka Kadeshi-balineya
kwa nzila ya chidunda cha Seili. 3 Zuwa lya
mwaluko lya mwezi wa kumi na imwe, mwaka
wa makumi gane, lowalawile Misili, Musa

nakawalonjela wanhu wa Isilaeli chila chinhu
Mkulu Nguluwi choyamlajize yawalonjele.
4 Nakadita ahyo hala du loimalile ngondo ya
kuwasumya mndewa Sihoni wa Waamoli yawele
yochikala kuli muji wa Heshiboni, na mndewa
Ogu wa Bashani nayawele yochikala kuli miji
ja Ashitaloti na Edileyi. 5 Musa nakawalonjela
wanhu malajizo ga Nguluwi mhela lonawali kuli
ubanzi wa keli wa lwanda lwa Yolodani kuli isi ya
Moabu.

Nakawalonjela ahi, 6 “Lotuwele kuli chidunda
cha Holebu*, Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe
nakatulonjela ahi, ‘Mikala kwa mhela wa kuhega
kuli chidunda achi. 7 Lelo muche hano mlu-
tilile na majendo. Mlute kuli isi ya vidunda vya
Waamoli na honhu hawele habehi na ibindi lya
Yolodani, kuli isi ya vidunda na kuli isi ya mibindi
ako Negebu na honhu ha mhwani, ena, mlute
mbaka kuli isi ya Kanaani na isi ya Lebanoni,
mbaka kuli lula lwanda lukulu lwa Eyufulate. 8 Isi
ayi yeng'ha ndiiwika hali hemwe. Lelo mlute
mkaihole isi ayo iwele heni Mkulu Nguluwi nandi-
laha kuwapa wasekulu wa hemwe Abulahamu na
Isaka na Yakobo na walelwa wa hewo.’ ”

### *Musa kanguhagula vilongozi (Kulawa 18:13-27)*

9 Musa nakawalonjela wanhu, “Nalotuwele
tung'hali kuchidunda cha Holebu, heni nandi-
walonjela ahi, ‘Mbuli ya kuwalongoza hemwe
ndo ng'hulu ng'hatu kusinda ludali lwa heni
ndiliyeka. 10 Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe,

* **1:6** Holebu Chidunda achi kahi changuzeleka kota ndo chidunda cha Sinai.

kawadita muwe wenji, lehano muwa wenji kota
nhondwe za kilanga. 11 Mkulu Nguluwi, Ngu-
luwi wa wasekulu wa hemwe, yawadite mon-
jezeche mala elufu mzidi ya vila vyomuwele
sambi na kuwatambichiza kota navyoyelahile!
12 Ila heni ndiliyeka ndoweza ndaze kuhola mbuli
azo za itunyo lya hemwe na kilewa kwa hemwe?
13 Mhagule kulawa kuli chila nhanzi ya wanhu
wawele na luhala na nyhala na uwanzi leka ndi-
wawiche wawe vilongozi wa hemwe.’ 14 Hemwe
namkunda na mnyidichila ahi, ‘Mbuli youlonjile
ndo inoga.’ 15 Ahyo nandiwahola wala vilon-
gozi wa hemwe wawele na luhala na uwanzi
wawele ndo muwahagule kulawila kuli nhanzi
za hemwe, nandiwawika wanji wawe vilongozi
wa hemwe kuli vilundo vya wanhu elufu imwe
na vilundo vya wanhu miya imwe na vilundo
vya wanhu makumi gahano na vilundo vya
wanhu kumi. Nandiwahagula kahi vilongozi
wang'hangala wanji kulawa chila nhanzi.

16 “Mhela wuwo nandiwapa vilongozi wa
hemwe malajizo aga, ‘Mhulichize nongwa za
wang'holozenu. Mtaguse kwa hachi hali nongwa
za wang'holozenu, hihyo du na kilewa kwa
wajenzi walingikala hamwe na hemwe. 17 Mleche
kumganilila munhu yoneche kuli kulavya
utaguso, mowahulichiza ne kubagula wawele
na lufufu ne wazunwa. Mleche kumdumba
munhu, mina hemwe moganigwa kutagusa
honhu ha Nguluwi. Wone kuwe na nhaguso iwele
ng'hulu kwa hemwe, moigala kwa heni, nani
ndoihulichiza.’ 18 Mhela wuwo nandiwalajiza
mbuli zeng'ha nazomganigwe kudita.

### *Waisilaeli wangulema kwinjila kuli isi yowelagane*
### *(Hisabu 13:1-33)*

19 “Lelo kota Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hetwe, navyoyatulonjele, natwaluka majendo
kulawila kuli chidunda cha Holebu natukola
kuli hala kuchiwala hagazi hakudumbiza, kota
homuhawene kwa kuwinza nzila ilinguluta isi
ya vidunda vya Waamoli. Natufika Kadeshibalineya,
20 heni nandiwalonjela, ‘Lelo mfika kuli
isi ya vidunda vya Waamoli iwele ndo Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hetwe, yalingutupa. 21 Mlole,
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, kaiwika isi
ayi hali hemwe. Mwinjile mkaihole kota Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa wasekulu wa hemwe navyoyawalonjele.
Mleche kudumba na kisinza!’

22 “Hamba mweng'ha namuya behi na heni
namndonjela, ‘Tuwalajize wanhu watulongole,
wakailole isi, hamba wahiluche kutuzelesa nzila
inojile ya kuwinza na miji jachi tojifika ako.’
23 Mbuli ayo nayoneka kota inoga kwa heni,
nandiwahagula wanhu kumi na weli, munhu
yumwe kulawila chila nhanzi. 24 Wanhu awo
nawaluta kuli isi ya vidunda, nawafika kuli ibindi
lya Eshikoli na kulilola chinyele. 25 Lowahiluche,
nawatugalila mafuza gamwe ga isi ayo na watulonjela
kota isi ayo yalingutupa Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hetwe, ndo inoga ng'hatu.

26 “Ila hemwe nahamuwinzile ilajizo lya
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, kwa
kulema kuluta kuli isi ayo. 27 Namng'ung'uta
mgati mwa mihema ja hemwe mlonga, ‘Mkulu
Nguluwi kangutuzudila mina nakatulavya kuli

isi ya Misili. Nakagana yatuwiche kuli moko ga
Waamoli leka watudumye. 28 Lekachoni tulute
ako? Tutweguche nhumbula kwa kudumba.
Nawatulonjela kota wanhu wa ako ndo wazidahe
na wawele ng'wemang'wema kusinda hetwe
vyotuwele na kota miji ja hewo migazi na
jizenjigwa lukanzi lufichile kilanga. Kahi
walonga kota nawawona wala walelwa wa Anaki
wawele ng'wemang'wema!'

29 "Ila heni nandiwalonjelani ahi, 'Mleche
kuwadumba wanhu awo. 30 Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hemwe, yawele yowalongola, heye
yuye kochitowa kwa chiwalo cha hemwe kota
navyoyaditile hali hemwe kula Misili, 31 na kula
kuchiwala komuwene vila navyoyawapapile
mmajendo gala geng'ha, kota vila mhaza
vyoyalingumpapa mwanage, mbaka namfika
aha.' 32 Ila hanga nandonga ago geng'ha, hemwe
nahamumkundile Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe, 33 ndo yawalongole mnzila na
kuwapalila honhu ha kuwasa hemwe. Nechilo
nakawalongolani kwa chiluli na nemisi kwa
ng'hungugu, leka kuwalajila nzila.

34 "Mkulu Nguluwi nakahulika kung'ung'uta
kwa hemwe, nakazudila, nakelaha yolonga,
35 'Kuduhu ne yumwe wa hemwe kuli lulelo alu
lwihile yokwinjila kuli isi yila inojile yondilahile
kuwapa wasekulu wa hemwe. 36 Kalebu mwana
wa Yefune, ndo heye yaliyeka yoyona, nani
ndomha isi ayo yoyaibijile iwe ya heye na
lulelo lwake kwa vila nayali yombinza heni
Mkulu Nguluwi kwa chila chinhu.' 37 Mkulu

Nguluwi nakazudila ng'hatu kwa heni kahi kwa
chiwalo cha hemwe nakalonga, ‘Na hegwe, Musa,
hukwinjila ng'oo kuli isi ayo. 38 Ila Yoshua mwana
wa Nuni, mtanzi wa hegwe, ndo yokwinjila
amo. Lelo mkangaze nhumbula kwa vila heye
kowalongoza wanhu wa Isilaeli leka wakaihole
isi ayo.’

39 “Hamba Mkulu Nguluwi nakatulonjela
hetwe tweng'ha, ‘Awo wana wa hemwe
womlingudumba kota wowa wapogozi wa
wang'honyo wa hemwe, ena, awo wawele
wadodo wawele hawavizelele kulekaniza
ganojile na gehile, awo ndo wokwinjila ako, nani
ndowapa hewo isi ayo iwe ya hewo. 40 Ila hemwe,
mgaluche na kuhiluka kuchiwala kulutila Bahali
ya Shamu.’

41 “Hamba namunyidichila, ‘Hetwe tumditila
gehile Mkulu Nguluwi, ila sambi toluta na ki-
towa kota Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe
vyoyatulajize.’ Ahyo, chila yumwe wa hemwe
nakewika goya kuza kitowa ngondo, mina nami-
jesa kota yahawele mbuli ndodo kuivaba isi ayo
ya vidunda. 42 Na heye Mkulu Nguluwi nakandon-
jela, ‘Walonjele hewo kota waleche kuza kitowa
kwa vila siwele hamwe na hewo, waleche kuluta,
wozalemwela hela kwa wang'honyo wa hewo.’
43 Lelo heni nandiwalonjela ahyo, ila hemwe nam-
libelenhuka ilajizo lya Mkulu Nguluwi namwin-
jila kuli isi ayo kwa kudadambala. 44 Aho,
Waamoli nawali wochikala kuli honhu aho ha
isi ya vidunda nawadulika nawawawinga hemwe
kota vila vyozilingudita nzuchi, ako nawawatowa
kulawila Seili mbaka Holima. 45 Lomhiluche,

nakumlilila Mkulu Nguluwi, ila Mkulu Nguluwi
nahawahulichize.
46 “Lelo namikala ako Kadeshi kwa mhela uhe-
jile.

# 2

### *Miyaka jimwenga kuchiwala*

1 “Hamba natuhinduka, natwinula majendo
kuchiwala kwa kukolela nzila ya Bahali ya
Shamu, kota Mkulu Nguluwi navyoyandonjele,
natulubaluba behi na chidunda cha Seili
kwa mhela uhejile. 2 Hamba Mkulu Nguluwi
nakandonjela, 3 ‘Namlubaluba kwa mhela wa
kuhega kuli isi ayi ya vidunda, lelo mgaluche
kukolela kasikazini. 4 Walajize wanhu awa,
“Mwahabehi kukola kuli isi ya vidunda vya Seili,
isi ya wang'holozenu walelwa wa Esau. Awo
wowadumbani, ila milolele, 5 mleche kitowa na
hewo kwa vila siwapani honhu honeche ha isi ya
hewo. Siwapani ne honhu hado ha kubiga. Isi ayo
ya vidunda vya Seili ndiwapa walelwa wa Esau
leka iwe ya hewo. 6 Homgana chilyo ama mazi
kulawila kwa hewo, iwagana mgule.” ’
7 “Lelo kota Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe navyoyawatambichize kuli chila mbuli
zomditile. Nakawalolela nalomwali mlubaluba
kula kuli chiwala chikulu. Nakawa hamwe na
hemwe miyaka aji jeng'ha makumi gane na
hamwisilwe ne chinhu choneche.
8 “Ahyo natulutilila na majendo ga hetwe,
natuwakola wang'holozetu na walelwa wa Esau
wawele wochikala Seili, natuheluka kahi na yila
nzila ya kibindi na honhu ha miji ya Elasi na

Esioni-gebeli. Hamba natuhinduka natuwinza
nzila ya kukolela kuli chiwala cha Moabu. 9 Mkulu
Nguluwi nakandonjela, 'Uleche kuwagaza wanhu
wa Moabu, na uleche kitowa na hewo mina siwa-
pani honhu honeche ha isi ya hewo. Ila honhu
aho ha Ali ndiwapa awo walelwa wa Loti hawe ha
hewo.' "

10 Aho katali ayo isi ya Ali nayali ya
Waemi, wawele na mong'ho na wawele
ng'wemang'wema kota Waanaki. 11 Kota vila
Waanaki, wanhu awa nawazeleka kahi kota
Walefayi, ila Wamoabu nawawachema Waemi.
12 Waholi kahi nawekala ako Seili aho katali, ila
walelwa wa Esau nawawawinga na kuwadumya,
hamba wawo baho nawekala aho kuli honhu ha
hewo. Waisilaeli nawadita kota ahyo kuli isi yila
iwele Mkulu Nguluwi nayawapele iwe ya hewo.

13 Musa nakalutilila kulonga, "Mkulu Nguluwi
nakatulonjela, 'Muche lelo, mloche kalwanda
ka Seledi.' Lelo natuloka kalwanda ka Seledi.
14 Miyaka makumi gadatu na nane najipuluta
kulawila kuka Kadeshi-balineya mbaka kuloka
kalwanda ka Seledi. Mhela awo, wanhu wa
chilundo chila wawele na miyaka ja kuhega kuza
kuli kitowa ngondo nawabagama kuwinza vila
Mkulu Nguluwi navyoyawalahile. 15 Mkulu Ngu-
luwi yuye nakawagaluchila leka yawadumye ako
kuli kambi, mbaka weng'ha wamale.

16 "Lelo wanhu awo weng'ha wawele na miyaka
ja kuhega kuza kuli kitowa ngondo lowabagame,
17 Mkulu Nguluwi nakandonjela, 18 'Lehano
moloka mbaka wa Moabu kwa kukolela isi ya
Ali. 19 Homfika kuli isi ya Waamoni, mleche

kuwatunya ne kitowa na hewo, kwa vila siwapani honhu honeche ha awo walelwa wa Amoni, iwe honhu ha hemwe. Hebu! Awo ndo lulelo lwa Loti, na ndiwapa ayo isi iwe ya hewo wawo.’ ”

20 Isi ayo yanguzeleka kahi kota isi ya Walefayi.
Walefayi nawali wochikala ako aho katali,
Waamoni nawawachema awo Wasamusumi.
21 Nawali wanhu wenji, wawele na mong'ho
na wawele ng'wemang'wema kota Waanaki.
Ila Mkulu Nguluwi nakawadumya lowafichile
Waamoli nawawele waiholile isi na kikala
amo honhu ha hewo. 22 Mkulu Nguluwi
nakadita kota navyoyawaditile wana wa
Esau, walinguchemigwa Waedomu, nawawele
wochikala kuli isi ya Seili. Nakawadumya Waholi
mhela Waedomu lowafichile ako, nawaihola isi
ya hewo na kikala amo mbaka lehano. 23 Waavi
nawali baho mwaluko wochikala kuli vijiji
vya hafungo mwa Mediteleniyani kuza mbaka
Gasa. Wakafutoli kulawila chihilwa cha Kilete
nawawadumya, nawekala amo honhu ha hewo.

24 Musa nakalutilila kulonga, “Hamba Mkulu
Nguluwi nakatulajiza, ‘Mwaluche majendo.
Mloche ibindi lya Alinoni. Heni ndimuwika
mmoko mwa hemwe Sihoni, mndewa wa
Waamoli wa Heshiboni na isi ya heye. Mumtowe
na kwaluka kuihola isi ya heye. 25 Lehano
ndokwaluka kuwadita wanhu weng'ha muisi
wawe wodumba na kuwa na lunhwinhwi kwa chiwalo cha hemwe, wohulika mbuli za hemwe na hewo wokakama na kudumba.

### *Waisilaeli wangumsumya mndewa Sihoni (Hisabu 21:21-30)*

26 “Lelo nandiwalajiza wasenga kulawila kuchi-
wala Kedemoti walute kwa mndewa Sihoni wa
Heshiboni na usenga awu ulinguya kwa kikala
goya. 27 ‘Utukundize tukole kuli isi ya hegwe.
Tokola mnzila na kulutilila ne kuhinduka kudilo
ne kumoso. 28 Chilyo cha hetwe togula kwa hegwe
na mazi ga kunwa kahi. Chotulanda du hetwe
ndo kukundizwa kukola kwa magulu muisi ya
hegwe, 29 tuloche lwanda lwa Yolodani na kwin-
jila kuli isi iwele Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hetwe yalingutupa. Walelwa wa Esau walingikala
Seili na Wamoabu walingikala Ali nawatukun-
diza kahi kukolela kuli isi ya hewo.’

30 “Ila Sihoni, mndewa wa Heshiboni, na-
hatukundize tukole kuli isi ya heye. Mkulu Ngu-
luwi, Nguluwi wa hemwe, nakamdita yawe na
nhumbula igagadale ng'hatu, leka tumsumye na
kuihola isi ya heye iwele tuikalila mbaka lehano.

31 “Hamba Mkulu Nguluwi nakandonjela,
‘Ulole, nyaluka kumuwika Sihoni na isi ya heye
mmoko mwa hemwe, mwaluche kuihola isi ya
heye.’ 32 Hamba Sihoni na wanhu wa heye
weng'ha nawoya kitowa na hetwe behi na mji
wa Yahasi. 33 Na heye Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hetwe nakamlavya, natumsumya heye na
wana wa heye na wanhu wa heye weng'ha.
34 Natuhola isi ya heye na kuwifyanga miji ja
heye jeng'ha, natuwakopola walume na wadala
na wana, nahatumlechile ne munhu yawele
mkomu. 35 Natuhola migongolo na lufufu lunji
lweng'ha natulufichile kuli miji. 36 Kwaluchila
Aloeli, muji uwele mgati mwa ibindi lya Alinoni
mbaka Gileadi, kuduhu muji woneche nawali

wimile mbaka natulemwa kuuhola. Mkulu
Nguluwi nakawika geng'ha mmoko mwa hetwe.
37 Ila nahatuihejelele isi ya Waamoni ama mfungo
mwa lwanda lwa Yaboki ne kuli miji ja isi ya
vidunda ne honhu honeche hala hawele Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, nayatulemeze.

# 3

### *Kusumigwa kwa mndewa Ogu (Hisabu 21:31-35)*

1 "Hamba natuhinduka, natuluta kuli nzila
ya kuluta Bashani. Mndewa Ogu nakalawa
na wanhu wa heye weng'ha kitowa na hetwe
habehi na muji wa Edileyi. 2 Ila Mkulu Ngu-
luwi nakandonjela, 'Uleche kumdumba, mina
ndimuwika mmoko mwako hamwe na wanhu wa
heye weng'ha na isi ya heye. Komditila kota navy-
oumditile Sihoni mndewa wa Waamoli nayekale
kula Heshiboni.'
3 "Lelo Mkulu Nguluwi nakamuwika mmoko
mwa hetwe Ogu mndewa wa Bashani na wanhu
wa heye weng'ha, natuwadumya nahaponile ne
munhu yoneche. 4 Natujihola miji jeng'ha ja
heye, kuduhu muji ne umwe uwele nahatuuho-
lile. Jeng'ha natujihola miji makumi sita, mina
honhu heng'ha ha Aligobu nahawele holongozwa
na Ogu mndewa wa Bashani. 5 Miji jeng'ha
aji najali na lugagala luwele na lukanzi lulutile
kuchanya, naluwele na lwizi lugazi na mhajilo.
Nakwali kahi na vijiji vinji navyali hela lugagala
luwele na lukanzi. 6 Natudumya chila chinhu ako,
natuwifyanga chila muji na kukopola walume na
wadala na wana kota navyotuditile kuli muji wa

mndewa Sihoni wa Heshiboni. 7 Ila migongolo
jeng'ha na lufufu natuhola hetwe.
8 “Mhela awo natuihola isi ayo ya wala wan-
dewa weli wa Waamoli nawawele wochikala ko-
lilawilaga isanya mwa lwanda lwa Yolodani, ha-
gati ha lwanda lwa Alinoni na chidunda cha He-
limoni.” 9 Wasidoni wanguchichema chidunda
acho Silioni, nawo Waamoli wanguchichema Se-
nili. 10 Musa nakalutilila kulonga, “Natujihola
miji jeng'ha jiwele muwegawega mwa chidunda
na kahi honhu heng'ha ha Gileadi na Bashani
mbaka Saleka na Edileyi, miji ja mndewa Ogu
ako Bashani.” 11 Mndewa Ogu yaliyeka ndo
nayaponile hali Walefayi na ndo nayali mndewa
wa Bashani. Chinhanda cha heye nachigongo-
manyigwa kwa chuma, nachali na utali wa mita
zine na ugazi wa behi ya mita mbili, kota vipim-
ilo navyoviwichigwe. Chinhanda acho ching'hali
kuli muji wa Waamoni wa Laba.

### *Nhanzi zikale kolilawilaga isanya mwa Yolodani*
### *(Hisabu 32:1-42)*

12 Musa nakalutilila kulonga, “Navyotuiholile
isi ayo, nandiwapa nhanzi za Lubeni na Gadi
honhu haluchile kasikazini mwa Aloeli behi na
Alinoni na nusu ya isi ya vidunda vya Gileadi
hamwe na miji jake. 13 Hamba nandiipa nusu
ya yila nhanzi ya Manase honhu haponile ha
Gileadi hamwe na Bashani yeng'ha nailongozwe
na Ogu, mina ndo honhu heng'ha ha Aligobu.”
Isi yeng'ha ya Bashani yanguzeleka kota isi ya
Walefayi. 14 Yaili munhu wa nhanzi ya Manase,
nakahola honhu heng'ha ha isi ya Aligobu, mina

ndo Bashani, kuza kuli mbaka wa Wageshuli na Wamaakati. Vijiji vyeng'ha nakavichema itagwa lyake, na mbaka lehano vyanguzeleka kota vijiji vya Hawoti-yaili.
15 Musa nakalutilila kulonga, “Wanhu wa lukolo lwa Makili wa nhanzi ya Manase nandiwapa Gileadi
16 na wanhu wa nhanzi ya Lubeni na Gadi nandiwapa isi yeng'ha kulawila Gileadi mbaka lwanda lwa Alinoni. Kusini nawabakana hagati ha lwanda na kasikazini nakwali na lwanda lwa Yaboki naluwele behi na isi ya Waamoni.
17 Ubanzi wa kolizinjilaga isanya isi ya hewo nayenela mbaka lwanda lwa Yolodani, kulawila ilamba lya Galilaya, ubanzi wa kasikazini kudulika kuza Bahali ya Mwino, mbaka kuli miduliko ja Pisiga ubanzi wa kolilawilaga isanya.

18 “Mhela wula nandiwapa walume wa nhanzi za Lubeni na Gadi na Manase ya kolilawilaga isanya, malajizo aga, ‘Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, nakawapani isi ayi muihole. Lelo hemwe muwele na mong'ho hali wang'holozenu, muwe muwichigwe goya kitowa ngondo, mloche lwanda lwa Yolodani muwele kumwando kwa wang'holozenu Waisilaeli.
19 Ila wadala wa hemwe na wana wa hemwe na migongolo minji ja hemwe, ahyo jopona kuli miji jondiwapele.
20 Muwatanze wang'holozenu Waisilaeli mbaka Mkulu Nguluwi hoyowadita wasindamale honhu hawo kota hemwe vyomsindamale, mina hewo nawo waihole isi iwele Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, kanguwapa kumwambu mwa lwanda lwa Yolodani. Homsinda ago moweza kuhiluka kuli isi ya hemwe, ayi muiholile ndiwapele.’

21 “Hamba nandimlajiza Yoshua, ‘Hegwe kona
kwa meho gako mbuli zeng'ha ziwele Mkulu Ngu-
luwi, Nguluwi wa hegwe, yawaditile wandewa
awa weli, Sihoni na Ogu. Lelo heye kowaditila
hihyo wandewa wa isi zeng'ha zoukola. 22 Mleche
kuwadumba mina Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, ndo kochitowa kwa chiwalo cha hemwe.’

## *Musa kangulemezwa kwinjila Kanaani*

23 “Mhela awo nandimdedeza Mkulu Nguluwi
ndilonga, 24 ‘Hegwe Mkulu, Mkulu Nguluwi ndi-
vizela kundajila heni chitumagwa wa hegwe
mwaluko hela wa ukulu wa hegwe na moko wa
hegwe uwele na mong'ho. Mina kuna mlungu
wachi ako kilanga ama kuli isi yoweza kudita
mbuli ng'hulu na za kububuwaza kota zouditile
hegwe? 25 Ndangukulanda ndoche lwanda lwa
Yolodani, ndiyone isi inojile kolizinjilaga isanya
mwa lwanda lwa Yolodani, ena, isi inojile ya
kunojeza ya vidunda, hamwe na vidunda vya
Lebanoni.’

26 “Ila Mkulu Nguluwi nakanzudila heni kwa
chiwalo cha hemwe, nakalema kunyhulichiza.
Hamba nakandonjela, ‘Ihega! Uleche kulonga
kahi mbuli ayi. 27 Ukwine mbaka kuli chinhem-
benhembe cha chidunda cha Pisiga, ulole goya
ubanzi wa kolizinjilaga isanya na kasikazini na
kusini na kolilawilaga isanya na koyona isi ayo,
ila hegwe huloka hebu alu lwanda lwa Yolodani.
28 Ila umhe Yoshua malajizo, umkangaze nhum-
bula na kumwimiza, mina heye ndo yowalongoza
wanhu awa mbaka kumwambu, kuihola isi youy-
ona.’

29 “Lelo natupona aha hawele na ibindi habehi
na Beti-peoli.”

# 4

*Kibatilila malajizo ga Nguluwi*

1 Musa nakalutilila kulonga, “Lelo hemwe
Waisilaeli mibatilile na kuwinza malajizo na
mizilo jondiwalanguse, leka mikale na kuihola isi
yila Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa wasekulu wa
hemwe, yoyawapele. 2 Mleche konjeza choneche
kuli ulonzi wondilinguwalajiza, na mleche kusa
chinhu, mibatilile malajizo ga Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hemwe, gala goyawapele. 3 Hemwe
namlola kwa meho genu mbuli zila Mkulu
Nguluwi zoyaditile hala Baali-peoli. Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, nakamdumya
chila yumwe wa hemwe nayamfugamile ayo
mlungu wa Baali-peoli. 4 Ila hemwe womuwele
mtanganiche kwa Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, mwa wakomu mbaka lehano.

5 “Mlole, ndiwalangusa malajizo na mizilo kota
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa heni, vyoyandajize,
leka mugawinze kuli isi yomluta kuihola.
6 Mibatilile na kugadita malajizo ago mina
homdita ahyo wanhu wa isi zinji howovizela
ago, wovizela kota hemwe ndo muwele na luhala
na nyhala, wolonga, ‘Twangukomya wanhu wa
isi ayi ng'hulu wana luhala na nyhala!’

7 “Kuduhu isi ng'hulu yoneche iwele mlungu wa
hewo kahabehi na wanhu, kota Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hetwe, vyoyawele behi na hetwe,
hotumlanda utanzi. 8 Na kuduhu isi yinji ng'hulu

yoneche iwele na malajizo na mizilo jitanganiche,
kota ajo jondiwalanguse hemwe wanhu zuwa ali
lya lehano.

9 “Ila milolele na mleche kusemwa mbuli
zila zomziwene kwa meho ga hemwe. Mbuli
azo zileche kulawa mnhumbula za hemwe kuli
mazuwa gose ga ukomu wa hemwe. Muwasimile
wana wa hemwe na wazukulu wa hemwe, 10 kwa
chiwalo cha zuwa lila nalomwimile hali Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, kula Holebu
hoyandojele, ‘Muwakungajize awo wanhu hali
heni, ndiwalonjele ulonzi wa heni leka welanguse
kundumba heni mazuwa gose ga ukomu wa hewo
na kuwalangusa wana wa hewo kudita ahyo.’

11 “Lelo namhejela na kwima hasi ha chila
chidunda chiwele mhela awo nachali chikwaka
chiluli nachifichile mbaka kilanga chigubiche
jiza na ng'hungugu ng'hulu. 12 Hamba Mkulu
Nguluwi nakalonga na hemwe hagati ha chiluli
acho, namuuhulika ulonzi woyalonjile ila na-
hamumuwene, namhulika hela lizi lyake. 13 Na
heye nakawadamlila ilagano lya heye nakawala-
jiza mbatilile na kuwinza jila mizilo kumi na-
joyandiche mli vibao vili vya maganga. 14 Mhela
awo yula Mkulu Nguluwi nakandajiza ndiwalan-
guse malajizo na mizilo jomlinguganigwa kudita
kuli isi yomlinguluta kuihola.

### *Makanyo galinguwala kufugamila jimalukolo*

15 “Nahamumuwene kwa meho Mkulu Nguluwi
hoyalonjile namwe kula kuchidunda cha Holebu
hagati ha chiluli, kwa chiwalo acho milolele
ng'hatu, 16 mleche kwajilila kwa kugongomanya

jimalukolo joneche ja kuhongola kwa kiwha-
niza kota mlume ama mdala [17] ama igongolo
lyoneche lila muisi ama chideje [18] ama kwa ki-
whana na igongolo lilingutambala hanyi ama
somba mmazi. [19] Milolele, leka mhela hom-
lola kilanga, isanya na nyelezi na nhondwe,
mleche kukwejigwa kuvifugamila ne kuviditila
chinhu choneche. Vinhu avyo Mkulu Nguluwi
nakavileka kwa wanhu weng'ha hasi ha kilanga.
[20] Ila hemwe ndo wanhu yoyawagombole Mkulu
Nguluwi kulawila Misili kuli itanuli lya chuma.
Nakawalavya ako leka muwe wanhu wa heye
kota vila vyomli lehano. [21] Kwa chiwalo cha
hemwe Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe,
nakanzudila heni, nakelaha kota heni siloka
lwanda lwa Yolodani kwinjila kuli isi yila inojile
yoyalinguwapa iwe uhalizi wa hemwe. [22] Heni
ndobagama kuli isi ayi na siloka lwanda lwa Yolo-
dani, ila hemwe mwa habehi kuluta kuihola isi
yila inojile. [23] Milolele ng'hatu mleche kusemwa
ilagano lila Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe,
loyaditile na hemwe na kiditila jimalukolo ja
kuhongola kwa kiwhaniza na chinhu choneche
chiwele Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe,
nakawalemeza kuwhaniza, [24] mina Mkulu Ngu-
luwi, Nguluwi wa hemwe, ndo chiluli chilingu-
lakaza, heye ndo Nguluwi yawele na fihi.

[25] “Homuwa mikale kuli isi ayo, homponda
wana na wazukulu muwe mlalile, wone
mwaluche kwajilila na kiditila jimalukolo ja
kuhongola kwa kiwhaniza na chinhu choneche,
namdite wihe hali Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe na kumzudiza, [26] lelo, heni lehano

ndanguvichema ulanga na isi vilole hali
hemwe, ndanguwalonjelani kota baho du
modumigwa ng'hatu kuli isi yomlinguluta
kuihola ako kumwambu mwa lwanda lwa
Yolodani. Hamchikala ako mhela uhejile,
ila modumigwa ng'hatu. 27 Mkulu Nguluwi
kowasambalula hali isi zinji na wanhu wachefu
hela wa hemwe wopona ako Mkulu Nguluwi
koyowawinjila. 28 Ako mojifugamila milungu ja
migodi na maganga jiwele jiditikwe kwa moko
ga wanhu na johajiwa jilola na hajilinguhulika
na hambe jilye ne kunusa. 29 Hamba kulawila
mumo mu isi mompala Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe, namwe momona wone mumpale kwa
nhumbula yeng'ha na muhe weng'ha. 30 Mbuli
azi zeng'ha hoziwafika aho hamwande, homgaya
momuhiluchila Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, na kumhulichiza. 31 Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hemwe, ndo Nguluwi yawele na
isungu, howaleka ne kuwadumya ne kusemwa
ilagano lila lyoyaliditile na wasekulu wa hemwe
kwa chilaho.

32 "Mijese ng'hatu kwa chiwalo cha gala
galawile katali, mbuli nazilawile hala hemwe
hamnapondigwa, kulawila zuwa lila Nguluwi
hoyamlumbile munhu muisi. Muuze kuli
isi yeng'ha, kulawila ubanzi umwe mbaka
wunji, wone mbuli ya kububuwaza kota
ayo mina ilawila ama kuhulikwa. 33 Ndaze,
wanhu wa isi mina wahulika lizi lya Nguluwi
lulonga kulawila hagati ha chiluli, kota hemwe
navyomhuliche, nakupona wakomu? 34 Ndaze,
kabaho Nguluwi yoneche yunji yajezile kuza

kuhola wanhu kulawila isi yinji, kota vila Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe? Nakadita hino
kwa kujezigwa na kwa kudita ulajilo na kwa
vinduzanduza na kwa ngondo na kwa moko
wa hegwe uwele na mong'ho na kwa ludali
lwake lukulu, nakambuza mbuli za kudumbiza
ziwele hemwe namzona kwa meho genu kula
Misili. 35 Hemwe namlajilwa mbuli azo, leka
mvizele kota Mkulu Nguluwi ndo yaliyeka
Nguluwi na haduhu yunji. 36 Nakawadita
mhuliche lizi lya heye kulawila kilanga leka
yaweze kuwalangusa kuhulichiza. Aha muisi
nakawadita mlole chiluli cha heye chikulu na
kuhulika ulonzi wa heye kulawila hagati ha
chiluli acho. 37 Kwa vila nakawagana wasekulu
wa hemwe, heye nakawahagula hemwe walelwa
wa hewo, nakawalavya yuye kuli isi ya Misili
kwa ludali lwake lukulu. 38 Nakawawinga hali
hemwe wanhu wa nhanzi ng'hulu na wawele
na ludali kusinda hemwe, leka yawegale na
kuwapani isi ya hewo kwa uhalizi, kota vyoiwele
lehano. 39 Lelo mkumbuche lehano na kuwika
mnhumbula za hemwe kota Mkulu Nguluwi ndo
Nguluwi kuchanya kilanga na hasi muisi, kuduhu
yunji. 40 Ahyo, mibatilile malajizo na mizilo ja
heye jondilinguwapa lehano leka mbuli ziditigwe
kwa hemwe goya, hamwe na walelwa wa hemwe
na kikala mazuwa menji kuli isi yila Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe kanguwapani iwe
ya hemwe mazuwa gose.”

### *Miji ja kubilimila kolilawilaga isanya mwa Yolodani*

41 Aho ndo Musa nakabagula miji jidatu
kolilawilaga isanya kwa lwanda lwa Yolodani,
42 kuwele munhu koweza kubilimila na kivisa
wone yamkopole munhu ne kunuwila nahawele
yamwihilwe. Munhu kota ayo koweza kubilimila
kuli muji umwe na kulohola ukomu wa heye.
43 Nakabagula muji wa Beseli muwegawega mwa
chiwala kwa chiwalo cha nhanzi ya Lubeni na
muji wa Lamoti kuli isi ya Gileadi kwa chiwalo
cha nhanzi ya Gadi na muji wa Golani kuli isi ya
Bashani kwa chiwalo cha nhanzi ya Manase.

### *Chilongole kwa malajizo ga Nguluwi*

44 Aga ndo malajizo Musa nayawapele Waisi-
laeli. 45 Aga ndo malajizo na mizilo na utaguso
Musa nayawalonjele Waisilaeli nalowalawile Mis-
ili, 46 nalowali kumwambu mwa lwanda lwa Yolo-
dani, kuli ibindi lya kumwando mwa Beti-peoli,
kuli isi naiwele ya mndewa Sihoni wa Waamoli,
nayalongoze muji wa Heshiboni, yula Musa na
Waisilaeli navyowamsumile nalowalawile Misili.
47 Nawaihola isi ya heye na ya mndewa Ogu wa
Bashani. Wandewa awo weli wa Waamoli nawa-
longoza ako kolilawilaga isanya mwa lwanda lwa
Yolodani. 48 Isi ayo nayenela kulawila Aloeli ha-
fungo mwa lwanda lwa Alinoni mbaka chidunda
cha Helimoni. 49 Hamwe na honhu heng'ha ha
ubanzi wa kolilawilaga isanya mwa lwanda lwa
Yolodani mbaka Bahali ya Mwino, mbaka kuli
miduliko ja chidunda cha Pisiga.

# 5

### *Mizilo kumi*
### *(Kulawa 20:1-17)*

1 Musa nakawachema Waisilaeli weng'ha,
nakawalonjela, “Mhulichize hemwe Waisilaeli,
malajizo na mizilo jondilingulonga na hemwe
lehano. Milanguse ago na kugawinza goya.
2 Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, nakadita
ilagano na hetwe kuchidunda cha Holebu.
3 Mkulu Nguluwi nahaditile ilagano alyo na
wasekulu wa hetwe, ila nakadita na hetwe
tweng'ha tuwele wakomu sambi baha. 4 Mkulu
Nguluwi nakalonga na hemwe mchilola ako
kuchidunda hagati ha chiluli. 5 Mhela awo heni
nanyima hagati ha hemwe na Mkulu Nguluwi,
nandiwalonjelani gala nagoyalonjile, kwa vila
hemwe namdumba chila chiluli na hamkwinile
kuchidunda.

“Mkulu Nguluwi nakalonga ahi 6 ‘Heni, ndo
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hegwe, ndikulavile
kulawila Misili, nakouwele mpogozi.

7 “ ‘Uleche kuwa na milungu jiyage ila heni.

8 “ ‘Uleche kiditila jimalukolo ja milungu ja
udesi, ama chihongoligwe chifandile na chiwele
kilanga ama kuli isi ama mmazi hasi ha isi.
9 Uleche kujifugamila milungu ja udesi ne ku-
jikolela mijito, kwa vila heni Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hegwe, nda Nguluwi yawele na fihi.
Ndanguwagaza wana kwa wihe wa wahaza wa
hewo, na lulelo lwa kadatu na lwa kane lwa awo
walingunzudila. 10 Ila ndanguwalajila igano lya
kwimilila maelufu ga wala wawele na igano kwa
heni na kibata malajizo ga heni.

11 “ ‘Uleche kulichema hela itagwa lya Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hegwe, mina heni ndo Mkulu Nguluwi sileka kumgaza yoneche yalingulichema hela itagwa lya heni.

12 “ ‘Udite Zuwa lya Kwesela na kuliwika liwe
lyelile, kota heni Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hegwe, vyondikulajize. 13 Mazuwa sita ukole mi-
jito na udite mbuli za hegwe zeng'ha, 14 ila zuwa
lya saba ndo zuwa lya kwesela kwa chiwalo cha
heni Mkulu Nguluwi. Zuwa alyo hegwe uleche
kukola mijito joneche, ne mwanago ne mhinza wa
hegwe ne mpogozi wa hegwe mlume ama mdala
ne isenga lyako ne idogowi lyako ne igongolo lya
hegwe lyoneche ne mjenzi yawele mgati mwa
lugagala lwako, leka mpogozi wa hegwe mlume
na mdala wesele kota hegwe vivila. 15 Uleche
kusemwa kota hegwe nawali mpogozi kuli isi ya
Misili, nani Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hegwe,
nandikulavya ako kwa moko uwele na ludali na
mong'ho, ndo mina heni Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hegwe ndikulajiza kulidita liwe Zuwa lya Kwe-
sela.

16 “ ‘Wahulichize mhaza na mayako, kota vila heni Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hegwe vyondikulajize, udite ahyo leka wikale miyaka minji na mbuli za hegwe ziditigwe goya kuli isi yondilingukupa.

17 “ ‘Uleche kukopola.

18 “ ‘Uleche kuwasa na mdala ama mlume wa munhu yunji.

19 “ ‘Uleche kuhiza.

20 “ ‘Uleche kulavya ulolezi wa udesi kwa yawele habehi na hegwe.

21 “ ‘Uleche kumgana mdala wa munhu yawele habehi na hegwe ne kuigana ng'handa ya heye ne mgunda wa heye ne mpogozi wa heye mlume ama mdala ne isenga lya heye ne idogowi lya heye ne chinhu choneche choyawele nacho.’

22 “Awo ndo ulonzi uwele Mkulu Nguluwi nawoyawalonjele wanhu weng'ha kwa lizi ng'hulu kulawila kuli chiluli na yila ng'hungugu idinyile jiza totolo. Nakawalonjela lonamwali mikungajize kula kuchidunda na honjeze aho mzilo wunji. Hamba nakandika mchanya mwa vibao vili vya maganga, nakamha.

### *Wanhu wangudumba (Kulawa 20:18-21)*

23 “Mhela nalomhuliche ayo lizi kulawa hagati ha lila jiza, kuchanya kwa chila chidunda nachali chikwaka chiluli, vilongozi weng'ha wa nhanzi za hemwe na wasekulu nawambuyila.
24 Hemwe namlonga, ‘Mhulichize! Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, nakatugubulila ukulu wa heye, tuhulika lizi lya heye kulawila hagati ha chila chiluli. Lehano natumona Nguluwi yolonga na wanhu, na heye munhu nahabagame ila nakalutilila kikala!
25 Ila ya choni kiwika hali nongwa ya kubagama kwa kulakazwa na chila chiluli chikulu? Hotuhulika kahi lizi lya Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, tobagama!
26 Ndaze, ndo munhu wachi nayahuliche lizi lya Nguluwi yawele mkomu kulawa hagati ha chiluli kota vyotumhuliche hetwe hamba nakapona mkomu?
27 Musa, ulute habehi kuhulichiza geng'ha goyolonga Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, hamba

uye kutulonjela mbuli azo zeng'ha zoyokulonjela.
Hetwe togahulichiza na kugadita.'
28 "Mkulu Nguluwi nakahulika ulonzi awo
weng'ha, nakandonjela, 'Nyhulika ulonzi
vyowokulonjela wanhu awa, geng'ha gowalonjile
ga goya. 29 Wone wawe na majesa kota aga
mazuwa geng'ha, nawawe wondumba na kibata
mizilo ja heni! Mbuli zeng'ha zahawele goya kwa
hewo wawo na walelwa wa hewo mazuwa gose.
30 Ulute ukawalonjele wahiluche kuli mihema ja
hewo. 31 Ila hegwe Musa wime aha habehi na
heni, ndokulonjela malajizo geng'ha na mizilo na
utaguso wouwalangusa, leka wadite ahyo kuli isi
iwele ndowapa iwe ya hewo.'
32 "Hemwe milolele mkadite kota Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe navyoyawalajize,
uleche kuleka kudita chila chinhu chilingu-
ganigwa. 33 Mowinza nzila zeng'ha Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, vyoyawalajize
kuwinza leka mbuli za hemwe ziditigwe goya na
mikale miyaka minji kuli isi yomuihola.

# 6

### *Ilajizo likulu*

1 "Aga ndo malajizo na mizilo na utaguso uwele
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe, nakanda-
jiza ndiwalanguse, leka mdite kuli isi yomlingu-
luta kuihola. 2 Mhela weng'ha womuwa wakomu,
mwanguganigwa kumdumba Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hemwe na kibatilila malajizo geng'ha
na mizilo jondilinguwapani hemwe na walelwa
wa hemwe leka mikale kwa miyaka minji. 3 Ahyo,

mhulichize hemwe Waisilaeli, milolele na ki-
batilila leka mbuli za hemwe ziditigwe goya na
konjezeka ng'hatu kuli isi ayo iwele na mboto
kota navyoyelahile Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
wasekulu wa hemwe.
4 “Lelo mhulichize hemwe Waisilaeli. Mkulu
Nguluwi, Nguluwi wa hetwe, ndo Mkulu Nguluwi
yumwe hela. 5 Namwe mumgane Mkulu Nguluwi
wa hemwe, kwa nhumbula za hemwe zeng'ha na
kwa muhe wa hemwe weng'ha na kwa mong'ho
wa hemwe weng'ha. 6 Na ulonzi awu wondilin-
guwalonjela lehano, muuwiche mnhumbula za
hemwe, 7 namwe muwalanguse wana wa hemwe
goya na kugalonga homchikalisa kuli ng'handa
za hemwe na homjenda mnzila na homuwasa
na homlilimka. 8 Mgakoweleze gawe ulajilo
mchanya mwa moko ga hemwe na kuwoha mvi-
hanga vya hemwe. 9 Kahi mgandiche mchanya
mwa vibatilila lwizi lwa ng'handa za hemwe na
mchanya mwa lwizi lwa lugagala lwa ng'handa za
hemwe.

### *Kukanyigwa kwa wanhu wohambe wahulichize*

10 “Kota vila Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, navyoyawalahile wasekulu wa hemwe,
Abulahamu na Isaka na Yakobo, heye kowa-
pani isi iwele na miji migazi na jidedemche
jiwele hemwe hamzenjile. 11 Ng'handa zowa
zimemile vinhu vinojile viwele hemwe hamvi-
wichile, kowa na mizimbo jiwele hajibawigwe na
hemwe na migunda ja zabibu na mizeituni jiwele
hemwe hamnyalile. Homuwa na chilyo choneche
chomlingugana, 12 milolele mleche kumsemwa
Mkulu Nguluwi yawalavile Misili nakomuwele

wapogozi. 13 Momdumba Mkulu Nguluwi, Ngu-
luwi wa hemwe, mowa vitumagwa wa heye na
kilaha kwa itagwa lya heye. 14 Mleche kuji-
winza milungu jinji na milungu ja wanhu wawele
habehi na hemwe, 15 ng'halazi ya Mkulu Nguluwi
ileche kuya kwa hemwe na kuwadumya ng'hatu
kulawa kuli isi, mina Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe yawele hagati ha hemwe, ndo Nguluwi
yawele na fihi.

16 “Mleche kumjeza Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe kota navyomumjezile ako Masa.
17 Mibatilile ng'hatu malajizo na utaguso na
mizilo ja Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe
jiwele heye joyalajize. 18 Mdite gawele na hachi
na ganojile hali Mkulu Nguluwi, leka mbuli
za hemwe ziditigwe goya. Moweza kuhola
isi yila inojile iwele Mkulu Nguluwi nakelaha
kuwapa wasekulu wa hemwe, 19 na mowawinga
wang'honyo wa hemwe kota Mkulu Nguluwi
navyoyawalahile.

20 “Mazuwa galinguya, wana wa hemwe
howowauza, ‘Malajizo na mizilo na utaguso
uwele Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe,
na kuwalonjela mdite, gana mana yachi?’
21 Hemwe mowedichila ahi, ‘Hetwe natwali
wapogozi wa Falao, mndewa wa Misili na
Mkulu Nguluwi nakatugombola kwa moko
wa heye uwele na mong'ho. 22 Kwa meho ga
hetwe twetwe, natumona Mkulu Nguluwi yodita
ulajilo na vinduzanduza vikulu vya kudumbiza
kwa kuwagaza Wamisili na mndewa wa hewo
Falao na wakulu wa heye. 23 Nakatulavya
Misili, nakatugala aha na kutupa isi ayi kota

navyoyelahile kota kowapa wasekulu wa hetwe.
24 Lelo Mkulu Nguluwi nakatulajiza kibatilila
malajizo aga na kumdumba kwa chiwalo cha
kutwamila hetwe leka tikale kota vyotulingikala
lehano. 25 Kahi towa tutanganiche wone tibatilile
malajizo hali Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hetwe,
kota navyoyatulajize.'

# 7

### *Nhanzi ihaguligwe na Mkulu Nguluwi (Kulawa 34:11-16)*

1 "Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe,
kowafichiza kuli isi yomluta kuzakikala na
kowawinga wanhu wenji kulawa kuli isi ayo.
Homkwinjila, kowawinga hali hemwe wanhu wa
isi saba ng'hulu na ziwele na mong'ho kusinda
hemwe, Wahiti na Wagiligashi na Waamoli na
Wakanaani na Wapelisi na Wahivi na Wayebusi.
2 Kahi, Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hemwe
hoyowawika mmoko mwenu, muwasumye
wanhu awo na kuwadumya ng'hatu, mleche
kuwika ilagano lyoneche na hewo na mleche
kuwonela isungu. 3 Mleche kihola na hewo, na
mleche kuwakundiza wana wa hemwe kihola na
hewo. 4 Homdita ahyo hewo wowajiliza wana wa
hemwe waleche kumfugamila Mkulu Nguluwi
na kuwadita wajifugamile milungu jinji, na
ng'halazi ya Mkulu Nguluwi yowagwila hemwe
hamba kowadumya kamwe. 5 Ila muwaditile
ahi, mobomola honhu ha kulavila nhambiko
na kugwisa mizengo ja maganga ga kufugamila
milungu ja hewo. Mizengo ja migodi ja Ashela
mojitema na kujisoma kwa chiluli jimalukolo ja

hewo ja kuhongola. 6 Mdite ahyo, leka muwe wa
chiuyeng'ha kwa Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe. Kuli wanhu weng'ha kuli isi yeng'ha,
Nguluwi nakawahagula hemwe leka muwe
nhanzi ya heye yuye.

7 "Mkulu Nguluwi nahawaganile hemwe na
kuwahagula kwa vila hemwe mwa wenji heko
kusinda wanhu wanji, hemwe namwali wachefu
kusinda nhanzi zinji kuli isi yeng'ha. 8 Ila kwa
vila Mkulu Nguluwi kanguwagana hemwe na
kangibata chilaho nachoyawalahile wasekulu wa
hemwe, ndo mina nakawagombola kwa moko
uwele na mong'ho na kuwalohola kulawa kuli
upogozi, kuli moko ga Falao mndewa wa Misili.
9 Lelo mvizele kota Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, ndo Nguluwi wa kitumbila. Kochibata
ilagano lya heye na kuwalajila igano lya kwimilila
kwa lulelo elufu lwa wala walingumgana na
kuwinza malajizo ga heye. 10 Ila holemwela
kuwagaza himahima wala walingumzudila.
11 Ahyo, muwe mchilolela na kibatilila malajizo
na mizilo na utaguso wondilinguwalajiza lehano.

### *Utambichizo kwa wala walinguhulichiza (Kukumbuchila 28:1-14)*

12 "Homuwinza malajizo aga na kugabatilila
na kugadita, Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
hemwe, kochibata ilagano lya heye na
hemwe, na kowalajila igano lya kwimilila
kota navyoyawelahile wasekulu wa hemwe.
13 Kowagana na kuwatambichiza, namwe
mokonjezeka na mowa na lulelo lwinji.
Kojitambichiza migunda ja hemwe leka muwe

na mbena ya kuhega na divai na mafuta ga
mzeituni, kowatambichiza kwa kuwapani
misenga na ming'holo minji kuli isi yawelahile
wasekulu wa hemwe kowapani hemwe.
14 Motambichizwa kusinda wanhu weng'ha
muisi. Kowa kuduhu mlume ama mdala ama
igongolo lya hemwe kowa mhende hali hemwe.
15 Mkulu Nguluwi kowosela hemwe matamwa
geng'ha na hamtamika matamwa goneche ga
kudumbiza kota nagomugule ako Misili, ila
matamwa ago kowapa wang'honyo wa hemwe.
16 Muidumye nhanzi yoneche Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa hemwe, koiwika mmoko ga hemwe
na mleche kuyonela isungu. Mleche kufugamila
milungu ja hewo, kwa vila mbuli ayi yowa ya
kuwagwiliza hemwe.

17 “Mleche kilonjelela mnhumbula za hemwe,
‘Wanhu awa ndo wenji kusinda hetwe, toweza
kuwawinga muisi?’ 18 Mleche kuwadumba,
mkumbuchile kota vila Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe, navyoyamditile Falao na isi yeng'ha
ya Misili. 19 Mkumbuchile matamwa gehile
mgawene kwa meho genu mwemwe na ulajilo
na kububuwaza na moko uwele na mong'ho na
ludali lukulu, uwele Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hemwe, nayawalohole hemwe. Ahyo
